

HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Temeke]

Simu: +255 22-292832
Fax: +255 22-2928137
Barua pepe: temeke@temekemc.go.tz
Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi
92 Barabara ya Mandela/Taifa
S.L.P: 46343,
15833 - DAR ES SALAAM,

Kumb Na. TMC/MD/E.5/1/13

Tarehe: 07/10/2020

NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke alipokea kibali cha ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi Chenye Kumb.Na.FA. **170/374/01/77** cha tarehe **26 Agosti, 2020** kwa ajili ya kuajiri Mtendaji wa Mtaa Daraja la III nafasi 1.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi iliyoainishwa katika tangazo hili, kama ifuatavyo:

1.1 MTENDAJI WA MTA A DARAJA III NAFASI (1)

1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Mtaa.
- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Mtaa.
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Mtaa
- IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Mtaa.
- V. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.

- VI. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Mtaa.
- VIII. Kusimamia Kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Mtaa.

SIFA/ ELIMU/ UJUZI

- Elimu ya kidato cha Nne (IV) au Kidato cha Sita (VI)
- Cheti (Astashahada) cha, Utawala, Sheria, Elimu ya jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi kutoka Chuo cha Serikali ya Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

NGAZI YA MSHAHARA

Ataanza mshahara **TGS B** kwa mujibu wa viwango vya Serikalini.

UMRI

Waombaji wote wanatakiwa wawe na umri usiopungua miaka **18** na usiozidi miaka **45**.

MASHARTI KWA UJUMLA

Maombi yote yawasilishwe yakiwa yameambatanishiwa na CV pamoja na nakala za vyeti vya kuhitimu elimu na mafunzo (vyeti vinavyoonyesha kiwango cha kufaulu na sio 'leaving certificate')

MUHIMU

Muombaji anatakiwa atume vyeti vyake halisi na halali kwani uhakiki utafanyika katika vyo alivyopitia pamoja na Baraza la Mitihani. Udanganyifu wowote ukibainika hatua za kisheria zitachukuliwa.

MAOMBI YATUMWE KWA ANWANI IFUATAYO:-

MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE,
S.L.P 46343,
DAR ES SALAAM.

Tangazo hili linapatikana pia katika wavuti ya Manispaa (www.temekemc.go.tz) na wavuti wa Serikali ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta, mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Jumanne tarehe **20/10/2020** saa **9.30 Alasiri**.

Imetolewa na



Lusubilo J. Mwakabibi
MKURUGENZI WA MANISPAA

MKURUGENZI WA
TEMEKE